Miongozo hii imetolewa na:
**Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini**,
S. L. P. 774,
Zanzibar, Tanzania

Kwa kupata nakala wasiliana na:
**Mradi wa Hifadhi ya Ghuba ya Menai**,
c/o Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini,
Zanzibar, Tanzania

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
**Mradi wa Elimu na Utafiti wa Wanyama wa Baharini**,
**Taasisi ya Sayansi za Baharini (IMS)**,
S. L. P. 668,
Zanzibar, Tanzania
au
**Mradi wa Hifadhi ya Ghuba ya Menai**,
c/o Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini,
Zanzibar, Tanzania

Kipeperushi hiki kimetolewa na:
**The Swedish Society for the Marine Environment (S-MAR)**
Box 6349
S-102 35 Stockholm, Sweden
www.smar.nu

S-MAR
Swedish Society for the Marine Environment

Layout by: www.webvisions-design.com, photos by: Per Berggren and Eva Stensland.

## MIONGOZO YA KUTAZAMA NA KUOGELEA NA POMBOO

Waendeshaji boti:

- Endesha boti kwa mwendo wa wastani. Epuka kubadilisha ghafla mwendo au mwelekeo wa boti. Usirudi kinyumenyume au kuzima na kuwasha mashine mara kwa mara.
- Likaribie kundi la pomboo kutokea nyuma au ubavuni na sio mbele yao.
- Usiwafukuzie pomboo, lakini waache waje wenyewe karibu na boti.
- Usiwazunguke pomboo au kuwakatiza mbele au katikati yao.
- Hakikisha pomboo wanapata njia ya kutokea kukiwa na boti zaidi ya mbili kwenye kundi moja la pomboo.
- Usimkurubie pomboo mwenye mtoto.
- Pomboo hupiga mikia yao juu ya maji, hukohoakohoa, huchupa au kuikimbia boti, kuashiria kuwa wanakerwa. Waache na badala yake tafuta wengine.




*Tourist boat in Menai Bay*

Kwa waogeleaji:

- Ingia majini kwa utulivu. Usiruke wala kupiga mbizi.
- Kuwa karibu na boti na shikilia boti au kamba pembezoni mwa boti.
- Usiwafukuzie pomboo, waache wakujie wenyewe.

# Miongozo kwa utalii wa pomboo, Zanzibar

Miongozo kwa ajili ya watalii na waendeshaji boti, Zanzibar

## UTAZAMAJI POMBOO

Utazamaji pomboo katika mazingira yao ya kimaumbile husisimua na ni njia moja ya kujifunza. Hata hivyo, tahadhari kubwa inapaswa kuchukuliwa ili kuepuka kuwakera wanyama hao, kitu ambacho kinaweza kubadilisha tabia zao za kimaumbile. Miongozo hii imetolewa kusimamia utalii wa pomboo ili kuhakikisha kuwa wanyama hao hawapati madhara au shinikizo na kuhakikisha kuwa pomboo wanaendelea kuwepo katika eneo walilolizoea. Utazamaji pomboo unaosimamiwa vizuri, huwa ni chanzo cha kawaida na endelevu cha mapato kwa jamii na ni njia mojawapo inayosaidia elimu na uhifadhi wa pomboo.



*1. Bottlenose dolphins (Tursiops aduncus)*

## POMBOO NI NANI?

Pomboo ni jamii ya wanyama wa baharini ambao huishi maisha yao yote katika maji. Kama walivyo wanyama wengine wa jamii hii (mammalia), pomboo ni wanyama wenye damu ya joto na huzaa mtoto mmoja kila baada ya miaka 3 hadi 4 ambao huwanyonyesha maziwa kwa miaka 2 hadi 3. Pomboo wana mapafu na huvuta hewa kupitia tundu zao za pua zilizoko juu ya vichwa vyao, hali hii huwafanya pomboo kuja juu ya maji kila baada ya dakika chache kuvuta hewa. Pomboo maarufu wanaoonekana katika bahari ya Zanzibar ni pomboo weusi (bottlenose dolphins) na pomboo weupe (humpback dolphins) (angalia picha na. 1&2), ingawa pomboo mdomo mrefu (spinner dolphins) pia ni maarufu katika bahari ya kaskazini ya kisiwa cha Unguja.

Pomboo ni wanyama wanaoishi kiukoo ambao hutumia muda wao mwingi wakiwa katika makundi makundi kuanzia pomboo wawili hadi mia kadhaa kutegemea aina yenyewe ya pomboo.

Pomboo hula aina tofauti za samaki na ngisi na hutumia milio maalumu ya sauti zao (kama mlio wa saa) kutafuta chakula. Vile vile pomboo huweza huwasiliana kwa kutumia miluzi. Kila pomboo mweusi huwa na mlio wa sauti maalumu ambao huwa ni kama kitambulisho chake, inayomtofautisha na pomboo wengine.



*2. Humpback dolphin (Sousa chinensis)*

## TABIA ZA KIMAUMBILE ZA POMBOO

Pomboo mara nyingi hujihusisha katika tabia za kijamii. Hupenda kuchezacheza kwa kugusana miili yao kwa kutumia mapezi yao ya ubavuni na vile vile huonesha tabia zinazoashiria hisia za kijinsia.

Pomboo wanapokuwa wanakula hutumia muda mfupi sana juu ya maji. Na wanapozamia kutafuta chakula, kawaida huinua mikia yao kuashiria kwamba wanakusudia kuzamia na kukaa muda mrefu chini ndani ya maji.

Tabia ya kuashiria kuwa wanasafiri huonekana pale wakati pomboo wanaogelea katika mwendo wa wastani katika mwelekeo mmoja kutoka eneo moja kwenda jengine. Kwa kawaida pomboo wanaposafiri huwa hawajihusishi na kitendo cha kutafuta chakula wala tabia yo yote ya kijamii.

Pomboo hupumzika kwa kubaki na kutulia katika eneo moja bila kuonesha ishara ya kula au kusafiri. Hutembea na kuzunguka taratibu wakiwa katika kikundi kimoja bila kutawanyika sana, hujitokeza juu taratibu kuvuta hewa wakati wamebakia katika eneo moja kwa muda mrefu.

## TABIA AMBAZO HUASHIRIA KUKERWA

Pomboo wenye watoto na walioshughulika na kula kwa kawaida ni rahisi sana kukerwa na boti na waogeleaji. Tabia zifuatazo huashiria kukerwa kwa pomboo:

- Kupiga mikia yao juu ya maji
- Kutoa sauti za kukohoakohoa
- Kuikimbia boti kwa mwendo wa kuruka
- Kuinua ghafla mikia yao juu na kuzamia
- Kukimbia ghafla kwa kundi zima

Utaratibu wa kila siku wa maisha ya pomboo unaweza kuathiriwa kwa; kelele za mashine, uendeshaji ovyo wa boti na uogeleaji mbaya. Haya yanaweza kupunguza muda wa pomboo wa kunyonyesha, kula na kutafuta mawindo, kuwasiliana baina yao na kutambua eneo walipo. Hii inaweza pia kuwalazimisha wanyama hao kuhamia maeneo duni. Kero hizi zinaweza kuwa na athari mbaya kwa maisha ya kila siku ya pomboo na athari za muda mrefu kwa ustawi wa pomboo katika bahari ya Zanzibar.

## KUZINGATIA USALAMA KWANZA

Vile vile kuna masuala ya usalama kwa wageni wanaotembelea pomboo ambayo yanapaswa kuzingatiwa. Wenye boti ni lazima wahakikishe kuwa vyombo vyao vinastahiki kutumika katika shughuli za kubeba wageni na vina vifaa kamili vya usalama ikiwemo mashine ya akiba.

Pomboo ni wanyama wasiofugwa na wakati wowote wanaweza kusababisha madhara kwa binadamu wanapochokozwa. Watalii ni lazima walitambue hili na waache pomboo wawajie wao wenyewe.